**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 31 Mei, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

108. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali inahimiza kina mama kujifungua katika vituo vya afya. Kwa kuwa katika kituo cha Afya Kiongwe, kuna wahudumu wawili tu wa mama na mtoto na ikifika saa 10 jioni, kituo kinafungwa na hata akitokea mzazi anayetaka kujifungua hulazimika kujifungulia nyumbani.

(a) Ni lini wataongezwa wahudumu wa mama na mtoto ili waweze kupanga ratiba ambayo itaondoa tatizo hilo.

(b) Likitokea tatizo wakati wa kujifungua nyumbani kwa kukosa mhudumu kituoni, ni nani atawajibika.

(c) Je, ni lini atapatikana daktari wa ziada angalau kumsaidia daktari aliyepo.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

154. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni)-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Miaka ya hivi karibuni kumejitokeza wimbi kubwa la uvamizi wa viwanja vya wazi na vile vya michezo kwa baadhi ya watu kujenga makaazi, maduka ya biashara na ghala. Hali hii inapelekea watoto wetu kukosa maeneo ya kucheza na kukuza vipaji vyao, na kuwafanya watoto waende maeneo ya mbali kutafuta sehemu za kucheza, jambo linalohatarisha usalama wao.

Je, Wizara imechukua hatua gani ya kufuatilia na kuzuwia uvamizi huo katika maeneo yote ya wazi na maeneo ya michezo kwa visiwa vya Unguja na Pemba.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

15. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,Vijana, Utamaduni na Michezo:

Mpira wa miguu ni moja kati ya mchezo unaopendwa sana katika nchi mbali mbali duniani ikiwemo Zanzibar. Hata hivyo, kwa upande wetu Zanzibar, hadi leo kiwango cha mpira wa miguu kiko chini sana katika medali ya kitaifa na kimataifa huku tukifahamu kuwa mpira wa miguu ni ajira tosha kwa vijana.

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha vituo vya kuibua na kuendeleza vipaji vya vijana katika vijiji vyetu vya Unguja na Pemba.

(b) Ni lini Serikali itaajiri Kocha wa kimataifa kwa ajili ya kufundisha timu yetu ya taifa.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

67. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Katika kukabiliana na tatizo la uingizaji wa dawa, vipodozi na chakula visivyo na viwango kwa matumizi ya binadamu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Taasisi ya kukabiliana na tatizo hili. Hata hivyo, katika hali ya kusikitisha na kuogopesha bado bidhaa hizo zisizo na viwango zinaendelea kuingizwa nchini na kuleta taharuki kwa wananchi wengi.

(a) Je, ni kwa nini hadi hii leo wafanyabiashara wanaingiza dawa feki, vipodozi na vyakula wakati bidhaa hizo zinapitia Bandarini na havishushwi na kutolewa hadi wapate kibali cha taasisi husika.

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuzifungia kampuni ambazo zinaingiza bidhaa hizo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

114. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini.

Kwa kuwa mtandao wa ZAWA katika eneo la Fuoni Polisi umeathirika kutokana na matengenezo ya barabara.

Je, ni lini huduma hiyo itarejeshwa ili wananchi waendelee kupata maji safi na salama.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

99. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka sera na sheria nzuri za uwekezaji katika maeneo tofauti ya nchi yetu ikiwemo eneo la Fumba. Na kwa kuwa wawekezaji huwa wanavutika na miundombinu rafiki ili kufanya uwekezaji wenye tija kwao na kwa nchi yetu.

Je, katika kufanikisha vivutio hivyo, Serikali ina mpango gani wa kuitengeneza barabara inayotoka Kombeni kuelekea Nyamanzi mpaka Fumba Town.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

77. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika mitihani ya kitaifa ya mwaka 2020, wako wadau muhimu sana kama vile wamiliki wa magari waliosambaza mitihani pamoja na askari polisi ambao hawajalipwa stahiki zao hadi sasa na badala yake wamelipwa walimu tu waliosimamia.

(a) Je, Serikali inalijua jambo hili.

(b) Na kama Serikali inalijua hili, Je, ni lini italipa madeni hayo kwa wahusika hao.

89. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini)

-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Je, kuna mpango gani wa kudumu wa ugawaji wa uji kwenye skuli hasa ikizingatiwa kuwepo kwa shida ya uhakika yakupatikana kwake.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2021/2022.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**31 Mei, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**